



KNOWLEDGE
TRANSFER


Mwongozo wa mkulima Marigold

• Maandalizi ya Shamba

- » Mifereji husaidia umwagiliaji na kutoa maji yaliyozidi shambani
- » Matandazo ya asili au ya plastiki yanaweza kuwekwa ili kutunza unyevu na kupunguza ukuaji wa magugu
- » Simika miti kwa ajili ya kufungia siku 8-10 baada ya kuhamisha miche shambani
- » Mimea 16660 - 33330 kwa ekari (idadi ya mimea inaweza kubadilishwa kulingana na aina ya mbegu na msimu)



SWAHILI




• Uzalishaji wa miche


- ◆ Kuandaa udongo wa kuoteshea miche: Choma udongo kwa dakika 10 au anika udongo juani kwa nusu siku, kisha jaza kwenye trei/viriba




- ◆ Otesha/Sia mbegu na kulinda miche




- ◆ Hakikisha unyevu unakuwa sawa muda wote



- ◆ Punguza kiwango cha maji na ongeza muda wa kukaa juani siku 2-3 kabla ya kuhamishia miche shambani wakati wa alasiri



• Uwekaji wa mbolea



Kiwango kinachoshauriwa kulingana na uhitaji wa wastani wa virutubisho vya mimea na idadi ya mimea 26600 kwa hekta (10700 kwa ekari)
Badili kiwango kulingana na msimu, hali ya rutuba ya udongo pamoja na hali ya ukuaji wa mimea

• Njia jumuishi za udhibiti wa visumbufu zao/mimea



» Tumia mitego ya gundi ili kufuatilia mwenendo na kukamata wadudu kwa wingi



Kuzuia kuenea kwa magonjwa, mimea iliyoathirika, mazao yaliyozeeka na magugu lazima yaondolewe shambani na yaharibiwe.

Kata sehemu ya juu inayokua katika kifundo/pingili cha tano au siku ya 10 - 12 baada ya kupandikiza



Kubadili zao kila msimu kunapunguza uzalianaji wa wadudu sumbufu na magonjwa shambani na kurudisha rutuba ya udongo

• Njia jumuishi za udhibiti wa visumbufu zao/mimea na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu

» Badili makundi ya dawa (MoA) ili kuzuia kutengeneza usugu

» Mara zote soma kibandiko cha maelezo ya kiuatilifu na matumizi yaliyokusudiwa (zao na kisumbufu vilivyosajiliwa kwavyo)




Kiambato amilifu (AI)	MoA (jinsi inavyofanya kazi)	Utendaji kazi	Vidukari	Nzi weupe	Kiwavi	kiwavi (chora chora)	Utitiri mwekundu
Lambda-cyhalothrin	3A	TM	✓	✓	✓	✓	✓
Dinotefuran	4A	T	✓	✓		✓	
Spinosad	5	T			✓	✓	
Spinetoram	5	TM			✓	✓	
Abamectin	6	TM (kwa kiasi kidogo T)			✓	✓	✓
Thiocyclam oxalate	14	TM	✓	✓		✓	
Chlorantraniliprole	28	T			✓		
Flubendiamide	28	T			✓		
<i>Bacillus thuringiensis</i>	11A	M			✓		
<i>Azadirachtin (Mwarobaini)</i>	UN	Haijulikani	✓	✓	✓	✓	✓

Jinsi inavyofanya kazi (MoA) kulingana na mwongozo wa kamati ya kushughulika na usugu wa viuatilifu dudu (IRAC); TM= Tumbo (T)+Mguso (M); Inayoingia kwenye mfumo wa ndani wa mimea



Kiambato amilifu (AI)	MoA (jinsi inavyofanya kazi)	Utendaji kazi	Maelezo	Mnyauko bakteria	Madoa jani altenaria (ALS)	Ubwiri unga	Kuvu ya maua (BFB)
Dawa za fangasi zenye copper ndani yake	M 01	P	Kwa magonjwa ya bakteria :Tumia tu pale inapolazimu; usizidishe matumizi kuepuka usugu	✓	✓	✓	✓
Chlorothalonil	M 05	P		Tumia aina za mbegu zenye ukinzani au miche isiyo na magonjwa	✓	✓	✓
Mancozeb	M 03	P			✓	✓	✓
Azoxystrobin	11	P + C	Isizidi mara nne kwa msimu		✓	✓	✓
<i>Bacillus subtilis</i>	BM02	P		✓	✓	✓	✓

Jinsi inavyofanya kazi (MoA) kulingana na mwongozo wa kamati ya kushughulika na usugu wa viuatilifu dudu FRAC; P = kuzuia (Inafanya kazi kwa ufanisi ikitumika kabla dalili za ugonjwa hazijaonekana), C = Tibu



Vaa mavazi ya kujikinga

Hali ya hewa nzuri

Nozeli nzuri

Osha vifaa kisha oga baada ya kunyunyiza viuatilifu

<https://growhow.eastwestseed.com>

Hakimiliki ©2021 na East West Seed Foundation. Haki zote zimehifadhiwa.

Ushauri wa viuatilifu uliotolewa hapa umeandaliwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Wageningen na Kitengo cha Utafiti (WUR)